

**LEBA**

Nafasi za kazi mtandaoni kutatua changamoto ya ukosefu wa nafasi za kazi mionganini mwa vijana, asema Waziri **UK 3**

**DATA**

Kamishna wa Kulinda Data aongoza kampeni ya kitaifa ya uhamasisho kuhusu usalama wa Data **UK 5**

**BIASHARA**

Kenya yatafuta uwejezaji zaidi kutoka India kuimarisha sekta ya uzalishaji bidhaa na ustawi wa kiuchumi

www.mygov.go.ke

JUNI 20, 2023

# MyGov.

TOLEO No. 49/2022-2023

**TATHMINI YAKO YA WIKI****Uk 11****Serikali yatia saini muafaka kuanzisha Huduma ya Afya kwa Wote kaunti****NA MABEL KEYA-SHIKUKU  
(KNA)**

Shirika la Bima ya Afya, Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya (NHIF), hivi karibuni itababalishwa kuwa Hazina ya Bima ya Afya ya

Kijamii (SIF) huku Serikali ikijaribu kuzindua Huduma ya Afya kwa Wote (UHC) katika kaunti 47.

Kulingana na Waziri wa Afya Dkt Susan Nakhumicha, makubaliano tarayi yametiwa saini kati ya seri-

kali ya kitaifa na serikali za kaunti 47 ili kuzindua UHC nchini mara moja kupitia mchakato wa kina wa ushirikiano wa washikadu.

Dkt Nakhumicha anasema katika utaratibu huo mpya, ufadhilli wa vituo vya Ngazi

ya Kwanza, Pili na Tatu utaghamiwa kwa utaratibu unaofadhiliwa na umma na kwa uwezo wa mtu binafsi, huku Hospitali za Ngazi ya Nne na Tano zikifadhiliwa kupitia Bima ya Afya ya Jamii na Level Sita itafa-

dhiliwa kupitia Hazina ya Magonjwa Sugu na Bima ya Afya ya Jamii.

Katika tarifa ya pamoja iliyosomwa na mwenyelekiti wa Baraza la Magavana (COG) Ann Waiguru mwishoni mwa mukutano wa siku

mbili mjini Naivasha amba lengo lake lilikuwa kukagua uhusiano kati ya serikali na ushirikiano kati ya ngazi mbili za serikali, ngazi hizo mbili za serikali zilisema.

**ENDELEA UK 2****KAWI****Serikali yasaka mbinu kupunguza gharama ya maisha, bei za bidhaa**

Waziri wa Kawi na Petroli Bw Davis Chirchir anasema kwamba Wizara yake inaangazia mapato ya ndani na hatua nyinginezo za kupunguza gharama ya bidhaa za petroli

**NA FATUMA SAID(KNA)**

Serikali kwa wakati huu inaendelea na mikakati mbalimbali inayolenga kupunguza gharama ya mafuta ya petroli na hatimaye kupunguza gharama za maisha kwa raia wake.

Waziri wa Nishati na Petroli Bw Davis Chirchir aliambia kamati ya bunge la kitaifa kuhusu nishati kwamba wizara yake inaingatia njia zote zinazowezekana za kupunguza gharama ya bidhaa ili kujapata suluhu zinazoweza kuwafaidi Wakenya wote.



**Waziri wa kawi na Bidhaa za Mafuta Davis Chirchir ahutubia kamati ya Bunge Kuhusu Kawi wakati wa mukutano wa mashauriano ulioandaliwa katika English Point Marina, Mombasa.**

Akizungumza wakati wa kongamano la mashauriano lilifanywa na Kamati ya Bunge la Kitaifa kuhusu Kawi, Bw Chirchir alisema kuwa wizara hiyo inafanya uchunguzi wa mapato ya ndani na hatua nyingine za kupunguza gharama za bidhaa za petroli.

"Ongezeko la gharama za bidhaa za petroli husabishi sha mfumuko wa bei, lakini ni muhimu sana kuwa na vichocheo vya uchumi ili kukomesha kuathiriwa kwa

**ENDELEA UK 2****Sherehe za kuadhimisha Siku ya Kiangazi Duniani**

Waziri wa Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Misitu, Soipan Tuya (kushoto) abadilishwa stakabadi na Gavana wa Kitui Dkt Julius Malombe wakati wa uzinduzi wa mpango wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kaunti ya Kitui wakati wa maadhisho ya Siku ya Kiangazi Mwaka huu katika Waita, Mwingi Central. Picha: HISANI

**2017**

Mwaka ambapo tupo za KUZA ambazo hutambua washindi katika sekta ya utangazaji zilianzishwa

**4.4**

Idadi ya Wakanya amba wanakumbwa na ukosefu wa chakula kulingana na uchunguzi uliofanywa mnamo Februari 2023

**700B**

Thamani ya miradi ya ujenzi wa barabara ambayo serikali inaendesha nchini

**2,000**

Vijana amba wamejunga na mpango wa kitaifa wa ustawi wa vijai kufanya kazini za mtando (NOESDP)

**38**

Miaka ambayo FIDA imepigania haki za akina mama nchini

**186**

Kilomita ambazo wanawake katika Benane, Lagdera hutembea kutafuta huduma za kujifungua katika Garissa Level 5 Hospital.